The Baptist Tabernacle of Los Angeles

1329 South Hope Street, L.A. Civic Center

Mailing Address:
P. O. Box 15308
Los Angeles, CA 90015

Phone: (213) 744-9999

E-mail: rlhymersjr@sbcglobal.net

www.sermonsfortheworld.com

www.baptisttabernacle.com

Dr. R. L. Hymers, Jr.
Founding Pastor

Dr. Christopher L. Cagan
Pastor

Desemba, 2019

Rafiki Mpendwa:

Natamani ningekutumia barua ya Krismasi yenye furaha zaidi. Lakini, kwa kweli, yanipasa nikwambie kwamba mwaka mmoja na nusu uliopita kanisa letu lilipitia mgawanyiko ulio kuwa wa kutisha kwa kweli.

Jambo hili lilianza miezi kadha kabla ya mwaka uliopita. Aliyekuwa kiongozi wa mashemasi alianza kuwa na mikutano ya siri na Mchungaji mwingine. Wawili hawa walipanga mpango wa kuliharibu kanisa letu. Wawili hawa walipanga mipango ya kuanzisha kanisa lingine na waondoke na watu wengi iwezekanavyo kutoka kwa kanisa letu. Wakati nilipogundua jambo hili walikuwa wameendelea kiasi cha kwamba singaliweza kuzuia mgawanyiko.

Jambo hili lilianza wakati ambapo shemasi asiyeridhika alipojaribu kunihusisha katika "kupigana makonde naye." Nilipokataa kupigana naye, aliondoka kanisani. Muda mfupi wengine wakafuata. Mwenye kiti wa mashemasi aliweka picha za ponografia katika tovuti yake. Mmoja wa "waliokuwa wakilipasua" kanisa alijaribu kunisingizia kuhusiana na picha hizi, na polisi walihusishwa. Mwenye kiti wa mashemasi na mke wake wakaliacha kanisa letu.

Wakati huu, aliyekuwa kiongozi wa mashemasi akajitokeza hadharani katika upinzani huu. Aliliacha kanisa letu na akaanza kuwavuta watu wengi iwezekanavyo. Kwa sababu kiongozi huyu wa mashemasi alikuwa kiongozi kanisani kwa miongo mingi, watu wengi walimfuata na wakaliacha kanisa letu. Kufikia mwisho wa mgawanyiko, alikuwa amefanikiwa kuwaondoa zaidi ya nusu ya watu.

Wakati huo hali yangu ya afya ilidhoofika na sikuweza kuhubiri ibada zote mbili za Jumapili. Mwanafunzi wa chuo cha Biblia alihubiri asubuhi ya Jumapili hiyo. Lakini kwa sababu ya ukosefu wa usoefu hakuweza kusimama nami wakati ambapo wengi wa marafiki wake wa karibu walikuwa wameondoka kutokana na mgawanyiko. Februari 20 kijana huyu alifunja ushirika nami. Yeye na mama yake waliondoka kanisani na wakaanza kushiriki katika makanisa ya Kiinjilisti. Mambo haya yalikuwa magumu kwangu kwa sababu nilimtarajia kijana huyu kuwa rafiki wangu wa karibu. Februari 23, nilijiuzulu kuwa Mchungaji na Dkt. Christopher Cagan akawa ndiye Mchungaji mpya. Na niliteuliwa kama Mchungaji mstaafu. Nilikuwa mdhaifu kiazi cha kwamba sikuweza kuhudhuria huo mkutano. Machi 3, Dkt. Cagan alitangaza kustaafu kwangu na kuteuliwa kwake kama Mchungaji. Dkt. Cagan ni Mkristo adhimu ambaye nimewahi kumjua, kando na Mchungaji Wurmbrand. Bila uongozi wake kanisa letu halingeweza kupona

Lakini mambo mazuri yanaendelea kutendeka. Januari 26 lugha ya arubaini na moja iliongezeka katika tovuti yetu. Siku hiyo hiyo (Februari 26) "app" yetu iliweza kuunganishwa kwa rukono za iPhone na Android. Tangu wakati huo maelfu ya watu kote Ulimwenguni wameungana nasi kupitia hii "app," shukrani hasa kwa rafiki, Mwanamisheni kwa Wayahudi katika jiji la New York. Halafu lugha ya arubaini na mbili ikaongezeka – lugha inayotumika sana katika nchi ya Malawi katika bara la Afrika. Februari 23, Dkt. Cagan akateuliwa rasmi Mchungaji kiongozi nami nikateuliwa kuwa Mchungaji mstaafu.

TOVUTI YETU INATOA MAMIA YA MAHUBIRI YA NENO-KWA-NENO KWA LUGHA ARUBAINI NA MBILI KATIKA TOVUTI HII WWW.SERMONSFORTHEWORLD.COM.

Hata pasipo kusema, nilikuwa mdhaifu ma mgonjwa kutokana na machafuko haya. Namshukuru mke wangu – aliyesimama nami katika matatizo haya yote. Februari 27 hadi Machi 20 nilimchukua tukaenda naye katika likizo ndefu kupumzika kule Arizona. Machi 20, nilirudi kuhubiri Jumapili jioni na kufundisha Jumamosi jioni.

Kutoka wakati huo jumba letu la kanisa likawa linauzwa. Aprili 14 sherehe yangu ya kuzaliwa ya mwaka wa sabini na nane ikawa katika jumba letu la zamani. Mei 7 nilianzisha kikundi cha uanafunzi cha watu wachanga waliowaaminifu katika kanisa letu, nikitumia "Mlipuko wa Uinjilisti" kama kitabu cha mafundisho. Kutoka Mei 22 hadi Mei 29, Dkt. Cagan aliandamana na mke wangu pamoja nami akatupeleka maeneo ya San Francisco kutembelea kanisa letu la Kichina la Kibaptisti pamoja na Mchungaji wake mzuri. Pia tulikutana na Mike na Mona Riley, Mchungaji wa muda mrefu wa kanisa nililolianzisha kule jimbo la Marin. Mike alinitia moyo sana, na nilialikwa kusungumza katika siku kuu yao ya ukumbusho wa miaka hamsini katika kanisa lao. Wengine hawakuwa na huruma, lakini walinilaumu kwa kule kupasuka kwa kanisa letu, na wakasababisha niwe na uchungu zaidi.

Julai 28 tuliandaa sherehe kubwa katika kanisa letu kusherehekea siku ya kusaliwa ya sitini na sita ya Dkt. Cagan. Ni wakati huo ambapo kulitangazwa kwamba kanisa letu jipya la bonde la San Gabriel litaitwa, "Baptisti Tabenakulo ya Kichina maeneo makuu ya Los Angeles." Tumenunua jumba jipya kule na escrow itafungwa hivi karibuni.

Baadaye katika mwezi wa Julai nilimchukua Bi Hymers tukaenda likizo fupi kule mwambao wa bahari. Mke wangu, Ileana, bila shaka ndiye mke bora zaidi wa Mchungaji katika Dunia nzima. Mwanangu Robert Leslie pamoja nami tulimtuma yeye pamoja na wazazi wake wawili kwenda Israeli. Novemba 17 nilianza mfululizo wa mahubiri kila Jumapili asubuhi na jioni. Ndio wakati nilioweza kimwili kuhubiri ibada zote mbili za Jumapili kwa muda mrefu. Chini ya uongozi na bidii ya Dkt. Cagan, vijana wawili waliokoka, na wanafunzi wa Kichina kadha wameanza kuhudhuria kanisa letu. Dkt. Cagan ameiuza nyumba yake iliyo eneo la Los Angeles, na anatafuta nyumba nyingine karibu na jengo la San Gabriel. Tutalihamisha kanisa letu katika jengo jipya miezi michache ijayo.

Mgawanyiko wa kanisa unaonekana umeisha. Niliambiwa siku chache zilizopita, kule mji wa tumaini, kwamba saratani yangu inaonekana imepona. Dkt. Cagan, mke wangu pamoja nami tulisherehekea kwa kurudisha shukrani katika nyumba yangu tukiwa na vijana wangu na wajukuu wetu, na wengi wa wale waliosimama nasi wakati huu mkuu wa majaribu. Tulikuwa na wakati mzuri pamoja!

Na Bwana awabariki nyote! Tafadhali kumbuka kutuombea tunapolianzisha kanisa la Kichina!

Ninajivunia sana jamii yangu. Kutoka kushoto kuelekea kulia, Wesley, Leslie na mtoto Hana, mimi, Ileana akiwa na mtoto Sara, Mke wa Leslie Jin, mamake Ileana Linda na nduguye Erwin Cuellar.

Yesu Kristo aliye Mwokosi wetu asifiwe!

R. L. Hymers, Jr.,
D.Min., Th.D., Litt.D.
Wafilipi 4:13

"Naamini nitauona wema wake Mwenyezi-Mungu katika makao ya walio hai. Mtegemee Mwenyezi-Mungu! Uwe na moyo, usikate tamaa! Naam, mtegemee Mwenyezi-Mungu!" (Zaburi 27:13-14).

TOVUTI YETU INATOA MAMIA YA MAHUBIRI YA NENO-KWA-NENO KWA LUGHA ARUBAINI NA MBILI KATIKA TOVUTI HII WWW.SERMONSFORTHEWORLD.COM.